PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

PPAA




Toleo Na: 10 Julai - Septemba 2026

# BULLETIN

"UTATUZI WA MIGOGORO KWA HAKI NA WAKATI"



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## PPAA yashughulikia zaidi ya asilimia 80 ya rufaa Mwaka wa Fedha 2025/26

### ...Yaiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha

**MPENDWA msomaji wa Jarida la "PPAA Bulletin" karibu tena ujisomee Toleo la Kumi (10) la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA). Jarida hili ni moja kati ya njia inazozitumia PPAA katika mawasiliano yake ya kimkakati ya kuwahabarisha wadau wa ununuzi wa umma na umma kwa ujumla kuhusu shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu.**

Ninayo furaha kukuletea Toleo la 10 la PPAA Bulletin kwa kipindi cha Julai – Septemba, 2026, kwa lengo la kukuhabarisha shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi tajwa.

Mbali na kutekeleza jukumu lake la msingi la kushughulikia malalamiko na rufaa zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi tajwa, PPAA imefanikiwa kushughulikia zaidi ya 80% ya rufaa Mwaka wa Fedha 2025/26, kuwanoa wadau wa ununuzi juu ya matumizi ya Moduli ya usimamizi wa malalamiko na rufaa takriban 2,600 na kushiriki katika Kongamano la 10 la Ununuzi wa Umma mwaka 2026 lililofanyika jijini Arusha.

PPAA imewahimiza wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma kutumia Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) kuwasilisha malalamiko na rufaa zao PPAA pindi wanapoona hawakutendewa haki katika michakato ya ununuzi wa umma, yatoa elimu kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST kwenye maonesho ya Kimataifa ya Kilimo (Nanenane) jijini Dodoma.

Katika toleo hili, tumekuandalia habari zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya PPAA katika kufikia malengo iliyokusudia kwa kipindi cha miezi mitatu ikiwa ni pamoja na kushiriki maonesho ya Nanenane, Kongamano la Ununuzi wa Umma ikiwa ni moja kati ya jitihada za PPAA za kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi na umma kwa ujumla.

Karibu usome toleo hili la 10 la PPAA Bulletin ili ufahamu kwa undani PPAA na shughuli ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu (Julai – Septemba, 2026) na kuendeleza ushirikiano imara katika utoaji rufaa kwa ufanisi, wakati na kwa haki kwenye sekta ya ununuzi wa umma.

***#Kazi na Utu, Tunasonga Mbele.***

***Karibu Sana***

# PPAA yawahimiza wazabuni kutumia Moduli ya Rufaa ya Mfumo wa NeST



*Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma cha Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. Nelson Kessy akizungumza na waandishi wa habari pembezoni mwa Kongamano la 10 la Ununuzi wa Umma lililofanyika Julai 2026 jijini Arusha.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imewahimiza wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma kutumia Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) kuwasilisha malalamiko na rufaa zao PPAA pindi wanapoona hawakutendewa haki katika michakato ya ununuzi wa umma.**

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw, James Sando pembezoni mwa Kongamano la 10 la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2026 jijini Arusha, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma PPAA, Bw. Nelson Kessy amesema kuanza kwa matumizi ya moduli hiyo kuna faida nyingi kama vile kuokoa muda na gharama.

"Faida nyingine za wazabuni na taasisi nunuzi kutumia moduli ni pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji pamoja na kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu sahihi za malalamiko na rufaa zinazowasilishwa na wazabuni, na kuongeza ufanisi katika

> *Inaendelea ukurasa wa 2*

BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA
PPAA
Toleo Na: 10 Julai - Septemba 2026




BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Florida Mapunda

Mhariri
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

Wajumbe
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga
Aliko Mwaiteke

Katibu
Nelson Kessy

Mawasiliano:
Katibu Mtendaji
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz




# PPAA yawahimiza wazabuni kutumia Moduli ya Rufaa ya Mfumo wa NeST

utoaji wa uamuzi," amesema Bw. Kessy

Bw. Kessy ameongeza kuwa Mamlaka ya Rufani inawaelekeza wazabuni wote wa ndani na nje ya nchi kutumia Moduli ya kuwasilisha Malalamiko na Rufaa kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na kanuni zake pindi wanapoona hawakutendewa haki katika zabuni walizoomba.

Katika hatua nyingine, Bw. Kessy amesema PPAA inatoa huduma ya Mkutano kwa njia ya Mtandao "Video Conference" kwa wazabuni na Taasisi nunuzi walioshindwa kufika moja kwa moja katika Ofisi za PPAA kusikiliza mashauri.

Huduma ya Mkutano kwa njia ya Mtandao imetoa fursa ya kuwasikiliza wazabuni walioshindwa kufika PPAA kutokana na sababu mbalimbali na kuiwezesha Mamlaka ya Rufani kutekeleza jukumu lake la msingi la utatuzi wa migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa Umma.

"Tangu kuanza kwa matumizi ya 'video conference' tayari PPAA imewasikiliza wazabuni mbalimbali kutoka katika mataifa ya Afrika Kusini, Nigeria, Poland, India na China," amesema Bw. Kessy.

Kadhalika, Mamlaka ya Rufani inatarajia kuunganisha Moduli ya Malalamiko na Rufaa na mfumo wa Mahakama ya Tanzania ili kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wakati na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma ikiwa ni njia mojawapo ya kuimarisha matumizi ya teknolojia katika sekta ya ununuzi wa umma.

Naye mzabuni Peter Sarungi kutoka makundi maalumu alisisitiza sekta ya makundi maalumu ipewe kipaumbele zaidi katika uombaji wa zabuni na kufuatilia taasisi zilizotangaza zabuni ili wapewe taarifa kama wamepata zabuni au la ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi ikiwemo kutumia Moduli ya PPAA.

Matumizi rasmi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST yalianza Februari, 2025.

# PPAA yashiriki Kongamano la 10 la Ununuzi wa Umma

## ...Yawaita wadau kupata elimu matumizi ya moduli




*Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Dkt. Toba Nguvila akizungumza na watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) katika banda la maonesho wakati wa Kongamano la 10 la Ununuzi wa Umma Mwaka 2026 lililofanyika Julai jijini Arusha. Katika Kongamano hilo, Dkt. Nguvila alimwakilisha Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar (Mb.).*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeshiriki Kongamano la 10 la Ununuzi wa Umma Mwaka 2026 jijini Arusha.**

Kongamano hilo limewakutanisha wadau wa ununuzi pamoja na viongozi wa serikali kwa lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kuimarisha sekta ya ununuzi na ugavi nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando, Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi amewahimiza wadau wa ununuzi wa umma kutembelea banda la Mamlaka ya Rufani kupata uelewa juu ya majukumu na huduma zinazotolewa na taasisi hiyo hususan matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST.

PPAA imeshiriki maonesho yanayofanyika pembezoni mwa Kongamano hilo kwa lengo la kutoa elimu kuhusu mchakato wa ununuzi wa umma, uamuzi juu ya rufaa zinazotokana na kufungiwa kushiriki katika michakato ya ununuzi wa umma pamoja na uamuzi juu ya malalamiko yanayotokana na kushindwa kwa Afisa Masuuli kutoa uamuzi ndani ya muda uliowekwa.

Awali, akifungua Kongamano hilo kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, (Mb.), Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Dkt. Toba Nguvila amesema sekta ya ununuzi wa umma inahusisha sehemu kubwa ya matumizi ya fedha za serikali, hivyo kuna ulazima wa kuhakikisha fedha zote zinazotengwa zinasimamiwa kwa umakini mkubwa ili kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

Dkt. Nguvila amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika mfumo wa ununuzi wa umma ili kuongeza uwazi, kupunguza gharama za ununuzi, kuharakisha mchakato na kurahisisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma.

"Ununuzi wa umma na ugavi ni nyenzo ya kisera na kimkakati ya serikali kuchochea uzalishaji, ukuaji wa viwanda, kuongeza ajira, kuimarisha kampuni za ndani, kukuza ubunifu, na kuhakikisha maendeleo yanayopatikana yanawanufaisha Watanzania wengi zaidi," amesema Dkt. Nguvila.

Kongamano hilo la siku tatu limeanza tarehe 29 - 31 Julai, 2026 limewakutanisha wadau wa ununuzi zaidi ya 1,500 wakiwamo wakuu wa taasisi, maafisa masuuli, maafisa ununuzi, idara tumizi, maafisa sheria, wazabuni na taasisi binafsi.




*Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi akizungumza na mwandishi wa habari wa Televisheni ya Clouds, Bw. Paul James katika banda la maonesho la PPAA wakati wa Kongamano la 10 la Ununuzi wa Umma Mwaka 2026 lililofanyika Julai jijini Arusha.*

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 10 Julai - Septemba 2026

# Huduma za PPAA zamkosha Waziri Ulega




*Aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega (Mb.) ambaye sasa ni Waziri wa Katiba na Sheria, akimsikiliza Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi alipotembelea banda la maonesho la Mamlaka ya Rufani. Maonesho hayo yamefanyika pembezoni mwa Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2026 kuanzia tarehe 13 – 14, Agosti, 2026 jijini Dar es Salaam.*

**Aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega (Mb.) amefurahishwa na huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) hususan matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulukia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST.**

Waziri Ulega ameipongeza PPAA alipotembelea banda la mamlaka hiyo pembezoni mwa Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2026 wa tarehe 13 – 14, Agosti, 2026 jijini Dar es Salaam.

PPAA imeshiriki maonesho hayo kwa lengo la kutoa elimu juu ya huduma mbalimbali inazozitoa kwa wadau wa ununuzi wa umma hususan matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulukia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST.

“Hongereni kwa kazi nzuri ya kutoa elimu kwa wadau wenu hasa wakandarasi walioshiriki katika mkutano wa leo, endeleeni kufanya kazi hii nzuri ili kutimiza azma ya serikali ya kuwasogezea wananchi huduma kwa karibu zaidi,” amesema Mhe. Ulega.

Kwa upande wake Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi ambaye alimwakilisha Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando katika mkutano huo, alimweleza Waziri Ulega kuwa kuanza kwa matumizi ya Moduli ya kupokea malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST kumechangia kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi kwenye mnyororo wa ununuzi na ugavi.

“Mhe. Waziri matumizi ya moduli katika mnyororo wa ununuzi na ugavi yamechangia kutoa maamuzi kwa haki na wakati na kuwezesha miradi ya serikali kutekelezwa kwa wakati,” amesema Bi. Sayi.

Pamoja na mambo mengine, Bi. Sayi amemweleza Mhe. Ulega kuwa kwa sasa PPAA inatoa huduma ya Mkutano kwa njia ya Mtandao “Video Conference” kwa wazabuni na Tasisi Nunuzi walioshindwa kufika katika Ofisi za Mamlaka ya Rufani kwa ajili ya kusikiliza rufaa zilizowasilishwa.

“Huduma ya ‘video conference’ inatoa fursa ya kuwasikiliza wazabuni na Taasisi Nunuzi walioshindwa kufika PPAA na hivyo kuiwezesha Mamlaka ya Rufani kutekeleza jukumu lake la msingi la utatuzi wa migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa umma kwa haki na wakati,” ameongeza Bi. Sayi.

Awali akifungua Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2026 jijini Dar es Salaam, Waziri Ulega amewataka \ akandarasi wazawa na wakandarasi wote nchini kuhakikisha wanatekeleza miradi wanayoipata kwa weledi na ufanisi.

Aidha, Waziri Ulega ameongeza kuwa serikali imeandaa mikakati ya kuwasaidia wakandarasi wazawa na washauri elekezi ili waweze kunufaika kupitia miradi inayotolewa nchini na kuwataka watendaji wa Wizara ya Ujenzi kutoa ushirikiano na kuhakikisha wanatatua changamoto zinazowakwamisha wakandarasi wa ndani kupata miradi.

Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi umeongozwa na Kaulimbiu, “Dira 2025: Fursa na Wajibu wa Makandarasi katika Ujenzi wa Miundombinu Endelevu”.




*Aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega (Mb.) ambaye sasa ni Waziri wa Katiba na Sheria, akiwapongeza watumishi wa PPAA kwa huduma nzuri ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST alipotembelea banda la maonesho la Mamlaka Rufani. Maonesho hayo yamefanyika pembezoni mwa Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2026 kuanzia tarehe 13 – 14, Agosti, 2026 jijini Dar es Salaam.*

# PPAA yawanoa wakandarasi mazingira ya haki michakato ya zabuni za umma




*Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi akitoa wasilisho juu ya haki kwa wazabuni katika Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2026 ulioandaliwa na Bodi ya Makandarasi (CRB) tarehe 14, Agosti, 2026 jijini Dar es Salaam.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imewajengea uwezo makandarasi kuhusu mazingira ya haki katika mchakato wa zabuni za umma, ili waweze kudai haki zao pindi wanapoona hawakutendewa haki kwenye michakato ya zabuni za umma walizoshiriki.**

Wasilisho la PPAA limewasilishwa na Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi ambaye alimwakilisha Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando katika Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2026 ulioandaliwa na Bodi ya Makandarasi (CRB) tarehe 13 – 14, Agosti, 2026 jijini Dar es Salaam.

Bi. Sayi amesema ununuzi wa umma ni zaidi ya utaratibu wa kununua kazi za ujenzi, bidhaa au huduma; ni nyenzo inayochochea ukuaji wa Uchumi, ajira na kuhakikisha matumizi bora ya fedha za umma.

“Mazingira ya haki katika mchakato wa zabuni za umma yanahakikisha wazabuni wote wanatendewa kwa usawa, wanashindana kwa kutumia masharti yanayofanana, na maamuzi yote yanafanywa kwa kuzingatia sheria, kanuni na masharti ya nyaraka za zabuni,” amesema Bi. Sayi

Ameongeza: “Mazingira ya haki katika zabuni za umma ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050”.

Kadhalika, Bi. Sayi ameeleza kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inahitaji mfumo wa ununuzi wa umma unaozingatia misingi ya haki, uwazi, uwajibikaji na ushindani wa haki.

“Maamuzi ya PPAA yanaonesha kuwa mazingira ya haki si suala la kisheria pekee bali ni nyenzo ya maendeleo ya Taifa. Kupitia uchambuzi wa maamuzi yake (jurisprudence), PPAA imeendelea kujenga mfumo unaolinda haki za washiriki wa zabuni, unaoimarisha uwajibikaji wa taasisi nunuzi na unaoongeza imani ya sekta binafsi kushiriki miradi ya maendeleo,” ameongeza Bi. Sayi.

Bi. Sayi amewasihi makandarasi, washauri elekezi, taasisi nunuzi na wadau wengine kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi wa umma ili kuiwezesha serikali kuwa na mfumo wa ununuzi unaochochea ushindani, matumizi bora ya fedha za umma na utekelezaji wenye mafanikio wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Naye Bw. Steven Masangia, Msanifu wa Majengo wa Kampuni ya Ebenezer Architects Ltd, ambaye alishiriki katika mkutano huo, amesema makandarasi wamekuwa wakitekeleza mikataba, ila baadhi ya vipengele vya kwenye Masharti Maalum ya Mkataba yamekuwa yakiwabana na kupelekea baadhi yao kufilisika.

“Makandarasi hawalipwi ongezeko la riba, jambo ambalo limekuwa likituathiri kiuchumi. Tunapaswa kulipwa ndani ya muda uliowekwa kwenye mkataba ili kutuwezesha kutekeleza mikataba kwa ufanisi,” amesema Bw. Masangia.

Masangia ameitaka PPAA kuendelea kutoa elimu kwa wazabuni na makandarasi ili wasichanganye malalamiko/rufaa dhidi ya uamuzi wa ununuzi na migogoro inayotokana na utekelezaji wa mkataba baada ya mkataba kusainiwa.

Mkutano wa Mashauriano na Wadau wa Sekta ya Ujenzi umewakutanisha wadau takribani 1,000 na umeongozwa na Kaulimbiu, “Dira 2025: Fursa na Wajibu wa Makandarasi katika ujenzi wa Miundombinu Endelevu”.

# Waziri wa Fedha akoshwa na matumizi ya Moduli



*Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb) akiwasilikiliza watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma alipotembelea banda la PPAA kwenye Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba.*

**WAZIRI wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb) ameonesha kuridhika na usimamizi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) katika matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulukia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST.**

Balozi Omar ametoa pongezi hizo alipotembelea Banda la Maonesho la PPAA lililopo ndani ya Banda la Wizara ya Fedha tarehe 02 Julai 2026 kwenye Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba ambapo PPAA inaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya huduma na majukumu yake.

"Hongereni kwa kazi nzuri ya kutoa elimu kwa umma, nimejulishwa kuwa kwa sasa baada ya matumizi ya Moduli kuanza hakuna longolongo kwenye mashauri yatokanayo na michakato ya ununuzi wa umma, endeleeni kusimia vyema matumizi ya moduli," amesema Balozi Omar.

Kwa Upande wake Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi ambaye alikuwa anamwakilisha Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alimweleza Mhe. Waziri Balozi Omar kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya Rufani imepokea malalamiko takribani 158 yaliyowasilishwa kupitia Moduli hiyo na kuyashughulika kwa wakati kama Sheria ya Ununuzi wa Umma inavyoelekeza.

"Mhe. Waziri matumizi ya moduli yanasaidia taasisi za serikali na wazabuni/ wadau wa ununuzi kwa ujumla kuokoa muda, gharama, inaongeza uwazi na uwajibikaji, inawezesha utunzaji wa kumbukumbu na kuiwezesha PPAA kutoa hukumu kwa haki na wakati," amesema Bi. Sayi.

Pamoja na mambo mengine, Mhe. Balozi Omar ameielekeza PPAA kuendelea kutoa elimu zaidi kwa umma kuhusu majukumu yake na matumizi ya moduli ili kutoa fursa zaidi kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma kuendelea kudai haki zao pale ambapo hawakuridhishwa na michakato ya ununuzi wa umma.

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya Rufani imefanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 1,907 pamoja na watumishi 705 wa idara za ununuzi na sheria katika maeneo mbalimbali nchini katika kanda za Kaskazini, Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Kati, na Pwani pamoja na mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Njombe, Iringa na Mwanza.



*Mkuu wa Sehemu ya Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando katika banda la mamlaka hiyo lililopo ndani ya banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba ji.jini Dar es Salaam.*

# PPAA yashughulikia rufaa zaidi ya 80% kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

## ...Yaiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha
## ...Wadau ununuzi wa umma takriban 2,600 wafikiwa mafunzo matumizi ya moduli

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imefanikiwa kushughulikia rufaa zaidi ya 80% zilizowasilishwa katika Mwaka wa Fedha 2025/26 na kuzitolea uamuzi kwa wakati na kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha.**

Takwimu hizo zimetolewa na Mkuu wa Sehemu ya Sheria wa PPAA, Bi. Agnes Sayi kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando katika banda la mamlaka hiyo lililopo ndani ya banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam.

"Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, PPAA ilipokea na kushughulikia rufaa zaidi ya 80% na kuzitolea uamuzi kwa wakati, rufaa zilizosalia zimefanyiwa kazi katika mwaka huu wa fedha 2026/27," amesema Bi. Sayi.

Aidha, Bi. Sayi ameongeza kuwa baada ya serikali kuweka sharti la lazima kuwa ununuzi wa umma kufanyika kwa njia ya kieletroniki, PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) ilijenga Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika Mfumo wa NeST, na moduli hiyo imeanza kutumika tangu Februari 2025.

"Ili kuwawezesha wadau wa ununuzi wa umma kutumia moduli hiyo, PPAA imefanikiwa kutoa mafunzo ya matumizi ya Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika mfumo wa NeST kwa wadau wa ununuzi wa umma takriban 2,600 nchini," amesema Bi. Sayi na kuongeza kuwa mafunzo hayo yaliwahusisha wazabuni takriban 1,907 pamoja na watumishi wa umma 705.

Bi. Sayi ameongeza kuwa PPAA katika maonesho ya Sabasaba inatoa elimu juu ya uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa zinazotokana na mchakato wa ununuzi wa umma, juu ya rufaa zinazotokana na kufungiwa kushiriki katika michakato ya ununuzi wa umma pamoja na kuhusu malalamiko yanayotokana na kushindwa kwa Afisa Masuuli kutoa uamuzi ndani ya muda uliowekwa.

Maeneo mengine yanayotolewa elimu ni kuhusu malalamiko baada ya mkataba wa ununuzi kuanza kutekelezwa, uamuzi juu ya maombi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha rufaa nje ya muda uliowekwa, uamuzi juu ya maombi ya utekelezaji wa amri ya Mamlaka ya Rufani, uamuzi juu ya maombi ya kufuta uamuzi uliotolewa bila kusikiliza upande mwingine na uamuzi juu ya maombi ya kurejesha rufaa.

Maonesho ya Sabasaba kwa mwaka 2026 yanaongozwa na kaulimbiu: Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba, Fahari ya Tanzania.




*Mkuu wa Sehemu ya Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi akizungumza na waandishi wa habari katika banda la Mamlaka ya Rufani lililopo ndani ya banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam. Wengine ni watumishi wa PPAA.*

# PPAA yatumia Nanenane kuwaelimisha wadau kuhusu Ununuzi wa Umma




*Sehemu ya washiriki wa maonesho ya Kimataifa ya Kilimo, Mifugo an Uvuvi ya Nanenane wakihudumiwa na watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), wakati wa maonesho yaliyofanyika katika Viwanja vya Dkt. John Samwel Malecela, Nzuguni jijini Dodoma, Agosti, 2026.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imetoa elimu kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Nanenane mwaka huu jijini Dodoma.**

Akibainisha mikakati ya PPAA kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani, Bw. James Sando, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma PPAA, Bw. Nelson Kessy amesema mikakati yake ni kuwaelimisha wadau wengi juu ya matumzi ya moduli ya kupokea malalamiko na rufaa ili kutoa fursa kwao ya kujua njia za kudai haki zao pindi wanapoona hawakutendewa haki katika michakato ya ununuzi wa umma.

Bw. Kessy amesema taasisi hiyo imeweka kambi ndani ya banda la Wizara ya Fedha, kuanzia tarehe 1- 8 Agosti, 2026 kwa lengo la kuwaelimisha wazabuni na taasisi nunuzi namna ya kuwasilisha na kushughulikia migogoro ya zabuni za umma kwa njia ya kieletroniki ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na kuokoa muda na gharama.

"Kupita Maonesho haya ya Nanenane, PPAA tunaendelea kutoa elimu mahususi juu ya matumizi ya moduli ya malalamiko na rufaa iliyopo katika mfumo wa NeST pamoja na huduma mbalimbali kama vile uamuzi juu ya rufaa zinazotokana na kufungiwa kushiriki michakato ya ununuzi wa umma na uamuzi juu ya malalamiko yanayotokana na kushindwa kwa Afisa Masuuli kutoa uamuzi ndani ya muda uliopangwa kisheria," amesema Bw. Kessy.

Amesema maeneo mengine yatakayoangaziwa na PPAA katika utoaji wa elimu ni uamuzi juu ya malalamiko baada ya mkataba wa ununuzi kuanza kutekelezwa, uamuzi juu ya maombi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha rufaa nje ya muda uliowekwa, uamuzi juu ya maombi ya utekelezaji wa amri ya Mamlaka ya Rufani, uamuzi juu ya maombi ya kufuta uamuzi uliotolewa bila kusikiliza upande mwingine na uamuzi juu ya maombi ya kurejesha rufaa.

Amesema PPAA inaendelea kutumia maonesho hayo kuhamasisha matumizi ya moduli ya malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST kama njia ya kutekeleza kauli mbiu ya Kitaifa ya NaneNane 2026: "Tambua Soko, Ongeza Tija, Kutekeleza Dira 2050".



# Migogoro inayoepukika: Rufaa 171 zinafichua nini kuhusu ununuzi wa umma?



***Na Dkt. Gladness Salema,*** *Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ni taasisi inayojitegemea chini ya Wizara ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 112 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya Mwaka 2023.**

Kwa mujibu wa sheria hiyo, jukumu kuu la PPAA ni kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya malalamiko au rufaa zitokanazo na maamuzi ya maafisa masuuli wa taasisi mbalimbali za umma katika michakato ya ununuzi wa umma. Pia, ina jukumu la kupokea na kusikiliza malalamiko ya wazabuni ambao hawakuridhishwa na uamuzi wa kufungiwa (blacklist) na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).




*Kielelezo namba 1*

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kudumisha misingi ya utawala bora, ikiwemo haki na usawa pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye tija kwa taifa. Katika kutekeleza majukumu hayo, ununuzi wa umma una nafasi muhimu, kwa kuwa takribani asilimia 70 ya bajeti ya serikali hutumika katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kazi. Hivyo, utekelezaji madhubuti wa sheria, kanuni na miongozo ya ununuzi wa umma ni msingi muhimu wa kuhakikisha michakato ya ununuzi inazingatia haki, uwazi, ushindani na thamani ya fedha.

Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa mfumo huo wa kisheria na juhudi zinazoendelea za serikali katika kuimarisha usimamizi wa ununuzi wa umma, uchambuzi wa majalada 171 ya rufaa yaliyosikilizwa na PPAA kati ya mashauri yaliyowasilishwa kati ya mwaka 2019 na 2026 umeonesha migogoro mingi ya ununuzi wa umma iliyowasilishwa mbele ya mamlaka hiyo ingeweza kuepukika iwapo taratibu za ununuzi zingetekelezwa kwa usahihi na kwa kuzingatia matakwa ya sheria, kanuni na miongozo husika.

Hivyo, uzingatiaji wa sheria na utekelezaji sahihi wa taratibu za ununuzi ni muhimu kuzuia migogoro, kuongeza ufanisi wa michakato ya ununuzi na kuhakikisha serikali inapata thamani halisi ya fedha.

Zipo sababu tatu (3) za msingi zinazojitokeza mara kwa mara katika rufaa hizo. Kwanza ni namna zabuni zinavyotathminiwa, hii ndio sababu inayolalamikiwa zaidi katika ununuzi wa umma. Aidha mapungufu hayo ni kama ifuatavyo: Dosari katika tathmini zilitajwa katika rufaa 151 kati ya 171, rufaa 140 zilitokana na malalamiko kuhusu wazabuni kuondolewa kwa kutokidhi vigezo vilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni na malalamiko kuhusu tuzo ya zabuni au mzabuni aliyeshinda zabuni (rufaa 123) (Kielelezo Na. 1).

Baada ya sababu hizo tatu, malalamiko kuhusu ukidhi wa vigezo vya kiufundi (rufaa 71) na tathmini ya bei (rufaa 58) yanafuata. Sababu za kutofuata utaratibu nazo kiutaratibu zinajitokeza, zikiwemo: ukomo wa muda (rufaa 38), kushindwa kwa mzabuni kuwasilisha kwanza malalamiko kwa taasisi nunuzi (rufaa 31) na masuala yanayohusu mamlaka ya kusikiliza shauri (rufaa 27). Masuala ya mzabuni kufungiwa kushiriki katika ununuzi wa umma, dhamana ya zabuni, ukiukwaji wa taratibu na kufutwa kwa zabuni, kila moja imejitokeza katika rufaa zisizozidi 20.

Ni muhimu kutambua kuwa sababu hizi mara nyingi hujitokeza kwa pamoja katika rufaa moja. Hata hivyo, jambo linalojitokeza kwa kiasi kikubwa ni malalamiko kwamba vigezo vilivyoainishwa kwenye nyaraka za zabuni havikutumika kwa namna vilivyoainishwa. Hivyo, kuboresha hali hii kunahitajika udhibiti imara wa kufanya tathmini ndani ya taasisi nunuzi, pamoja na miongozo iliyo wazi zaidi kwa wazabuni wote.

Katika rufaa 56, taasisi nunuzi zilikiri, katika utetezi wake wa maandishi au wakati wa usikilizwaji wa rufaa, kuwa utaratibu uliotakiwa haukufuatwa ipasavyo. Hali hii inaweza kuashiria changamoto katika maeneo mawili. Kwanza,

# Rufaa 171 zinafichua nini kuhusu ununuzi wa umma?

huenda baadhi ya watumishi wa umma wanazijua sheria lakini hawazifuati. Pili, inaweza kuashiria kwamba mifumo ya mapitio ya ndani ya kisheria na ya kiununuzi kabla ya tuzo hayabaini kwa wakati makosa sahihi ambayo yangeweza kuzuiwa badala ya kusubiri hadi suala lifikishwe mbele ya Mamlaka ya Rufani.

Zabuni zilizopitwa na muda: Katika rufaa 14, taasisi nunuzi ziliacha muda wa uhai wa zabuni ukaisha bila kuongeza muda kwa mujibu wa sheria, na baadae zikaendelea na hatua za kutoa tuzo, majadiliano au kusaini mkataba. Katika mfano mmoja wa rufaa, Bodi ya Zabuni iliidhinisha tuzo na majadiliano yakakamilika baada ya muda wa uhai wa zabuni kuwa umeshaisha. Mamlaka ya Rufani ilibatilisha zabuni hiyo. Jambo hili linaonesha umuhimu wa taasisi nunuzi kufuatilia kwa ukaribu muda wa uhai wa zabuni.



Uhai wa zabuni unapokaribia kuisha, hatua zinazohitajika kisheria zinapaswa kuchukuliwa mapema kuhakikisha mchakato unaendelea ndani ya muda unaotambulika kisheria. Kushindwa kufanya hivyo kunaweza kuathiri uhalali wa hatua zinazofuata na kusababisha mchakato wa ununuzi kubatilishwa.

Kufungiwa kushiriki ununuzi wa umma: Ni rufaa 18 tu zilizohusu kufungiwa kwa baadhi ya wazabuni kushiriki katika ununuzi wa umma, madhara ya uamuzi huo kwa mzabuni yanaweza kuwa makubwa. Kampuni inapofungiwa, huzuiwa kushiriki katika ununuzi wa umma kwa kipindi maalumu.

Rufaa saba (7) kati ya hizo zilionesha dosari za kiutaratibu. Miongoni mwa changamoto zilizoonekana ni taarifa kutumwa katika barua pepe zisizo sahihi au zisizofanya kazi, muda wa kuwasilisha utetezi kutotolewa kwa ukamilifu, na hatua za utekelezaji kuchukuliwa kabla mzabuni hajapata fursa ya kujibu tuhuma dhidi yake. Katika baadhi ya mashauri, maamuzi ya kumfungia mzabuni yalitenguliwa kutokana na kutokuwepo kwa uzingatiaji wa haki ya kusikilizwa.

Hili linaonesha umuhimu wa kuhakikisha mchakato wa kumfungia mzabuni unazingatia haki ya kusikilizwa, taarifa sahihi, muda unaotakiwa wa kuwasilisha utetezi na taratibu zote zinazotakiwa kisheria. Utaratibu usio sahihi unaweza kumwondoa mzabuni katika soko la ununuzi wa umma bila kufuata kikamilifu misingi ya haki na hivyo kudhoofisha imani katika mfumo wa usimamizi wa ununuzi wa umma.

Mfumo wa mapitio ya kiutawala umewekwa kwa lengo la kuiwezesha taasisi nunuzi kurekebisha makosa mapema, kwa ufanisi na kwa gharama ndogo kabla suala halijafikishwa mbele ya Mamlaka ya Rufani. Hata hivyo, uchambuzi wa rufaa hizi unaonesha kuwa mfumo huo wakati mwingine hushindwa kutumika ipasavyo na pande zote mbili.

Rufaa 21 zilitupiliwa mbali zote au kwa hoja za awali, kwa sababu mzabuni hakuomba kwanza mapitio ya kiutawala kwa taasisi nunuzi, aliibua hoja mpya katika rufaa, au aliwasilisha rufaa nje ya muda ulioainishwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma. Malalamiko kadhaa ya msingi hayakusikilizwa kabisa. Kwa upande mwingine, katika rufaa nane (8), taasisi nunuzi zilishindwa kutoa uamuzi kuhusu maombi ya mapitio ya kiutawala ndani ya muda uliowekwa kisheria. Hali hii iliwalazimu wazabuni kusubiri hadi muda wa kisheria upite au kuchukua hatua zinazofuata kwa mujibu wa sheria. Kwa namna hiyo, suala ambalo lingeweza kutatuliwa kupitia mapitio ya ndani liliishia kuwa malalamiko rasmi mbele ya Mamlaka ya Rufani chini ya Kifungu cha 121 (2) (a) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Mamlaka ya Rufani inahimiza Kitengo cha Ununuzi kukagua kila taarifa ya tathmini kabla Bodi ya Zabuni haijaidhinisha tuzo. Afisa asiye mjumbe wa kamati ya tathmini athibitishe kuwa vigezo vya tathmini vilitumika kama vilivyoandikwa katika nyaraka ya zabuni, mzabuni aondolewe kwa kuzingatia sababu zilizoainishwa kwenye tathmini ya zabuni, na zabuni bado iko ndani ya muda wake wa uhai. kutoa mafunzo kwa kamati za tathmini kuhusu kutumia vigezo vilivyoainishwa na kutofautisha kasoro za msingi na kasoro ndogo. Kufuatilia tarehe za muda wa uhai wa zabuni na ziongezwe mapema. Hakuna uidhinishaji, majadiliano wala kusaini mkataba unaopaswa kufanyika kwa zabuni ambayo muda wake umeisha. Kutoa maamuzi kuhusu maombi ya mapitio ya kiutawala ndani ya muda wa kisheria.

Kabla ya kuchukua hatua za kufungia kampuni, kuhakikisha taarifa zinawasilishwa kupitia njia sahihi na zinazoweza kuthibitishwa, muda unaotakiwa wa kujitetea unatolewa, na kampuni inapewa fursa ya kusikilizwa kabla ya uamuzi wa mwisho kutekelezwa.

Kwa upande wa wazabuni, PPAA inahimiza wazabuni kutumia kwanza utaratibu wa mapitio ya kiutawala kwa taasisi nunuzi; na kuwasilisha hoja zote muhimu wakati wa mapitio ya kiutawala ili kutoa fursa kwa taasisi nunuzi kurekebisha makosa mapema; kuzingatia kwa umakini muda uliowekwa kisheria wa kuwasilisha rufaa ndani ya siku tano za kazi, kuhakikisha taasisi nunuzi zina taarifa sahihi na zinazofanya kazi za mawasiliano ili taarifa muhimu za mchakato ziweze kuwafikia kwa wakati.

Kwa kuwa makosa mengi ni ya kiutaratibu, yanajulikana mapema na mara nyingi wahusika hukiri makosa hayo, ni vyema ukaguzi makini ufanyike kabla ya tuzo na mapitio ya ndani yafanyike kwa wakati kuzuia migogoro mingi kufika mbele ya Mamlaka ya Rufani, jambo linalochelewesha miradi kuendelea mpaka shauri lisikilizwe.

*Itaendelea toleo lijalo*




*Meza kuu katika picha ya pamoja na washiriki wa Kongamano la Viwanda, Uwekezaji, Teknolojia na Uvumbuzi kwa Wanawake, Vijana, Wazee na Watu Wenye Mahitaji Maalumu wa mikoa ya Kanda ya Kusini lililoratibiwa na Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Septemba 2026 mkoani Lindi.*

# Makundi maalumu Lindi waaswa kuchangamkia fursa zabuni za umma

## ...Wanolewa kuhusu njia za kudai haki katika zabuni za umma

**WANAWAKE, vijana, wazee na watu wenye mahitaji maalumu wa mikoa ya Kanda ya Kusini wametakiwa kuchangamkia fursa zinazopatikana katika zabuni za umma ili kuongeza ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya taifa.**

Wito huo umetolewa na Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Lindi, Bi. Alusaria Mushi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mhe. Adam Malima katika Kongamano la Viwanda, Uwekezaji, Teknolojia na Uvumbuzi kwa Wanawake, Vijana, Wazee na Watu Wenye Mahitaji Maalumu wa mikoa ya Kanda ya Kusini lililoratibiwa na Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Septemba 2026 mkoani Lindi.

Bi. Mushi amesema serikali imeendelea kuweka mazingira bora ya kuwainua wananchi kiuchumi kupitia mifumo ya ununuzi wa umma ambapo mifumo hiyo imekuwa ikiwawezesha wazabuni kushiriki kwa haki na uwazi, na haki zao zimekuwa zikilindwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma.

"Sheria na kanuni zinaruhusu mtu au kikundi cha watu wenye mahitaji maalumu kupata fursa ya mkopo wa kategoria ya makundi maalum ambapo mmetengewa asilimia 30 kwa vijana, wanawake wazee na watu wenye mahitaji maalumu, sasa kazi kwenu wana-Lindi kuchangamkia fursa hiyo. Ila changamoto kubwa ya ninayoiona kwenu kama makundi maalumu si fursa, bali ni utayari wa kuchangamkia fursa hizo," amesema Bi. Mushi.

Aidha, Bi. Mushi ameitaka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kuendelea kuwajengea uwezo vijana, wanawake, wazee na wenye mahitaji maalumu uelewa juu ya haki zao katika michakato ya ununuzi wa umma pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kushughulikia malalamiko na rufaa.

"Naomba PPAA muendelee kuwajengea uwezo vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalumu ili kuwawezesha kujua namna ya kudai haki zao pale wanapoona hawakutendewa haki katika zabuni walizoomba serikalini, kwani baadhi yao wamekuwa waoga au hawajui mahali pa kudai haki zao," ameongeza Bi. Mushi.

Pamoja na mambo mengine, Bi. Mushi amewasihi washiriki wa kongamano hilo kuchangamkia fursa zinazotokana na ununuzi wa umma ili kuwawezesha kunufaika kiuchumi na kwa maendeleo yao binafsi na ya taifa kwa ujumla lakini zaidi kwa maendeleo ya Mkoa wa Lindi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Sehemu ya Usimamizi wa Mashauri wa PPAA, Bi. Violet Limilabo ambaye alimwakilisha Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando katika kongamano hilo, amesema PPAA imeendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu haki na wajibu wa wazabuni katika michakato ya ununuzi wa umma, hususan matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kushughulikia malalamiko na rufaa pale wanapoona hawakutendewa haki.

Bi. Limilabo ameongeza kuwa, elimu hiyo inalenga kuongeza uwazi, uwajibikaji na imani ya wadau katika mfumo wa ununuzi wa umma, huku ikichochea ushiriki wa makundi mbalimbali katika shughuli za kiuchumi.

"Kwa sasa PPAA inapokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kupitia Moduli ya usimamizi wa Malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST, matumizi ya Moduli hiyo yameleta manufaa mbalimbali ikiwemo kuokoa muda, kupunguza gharama, kuongeza uwazi na uwajibikaji pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi za malalamiko na rufaa zinazowasilishwa na wazabuni," amesema Bi. Limilabo.

Kongamano hilo limewakutanisha takribani wanawake, vijana, wazee na watu wenye mahitaji maalumu 150 na kutoa fursa ya kujifunza, kubadilishana uzoefu na kujenga mitandao ya kibiashara itakayowawezesha kutumia fursa za uwekezaji, teknolojia na ubunifu zinazotangazwa na serikali hususani fursa zinazopatikana katika Mkoa wa Lindi.

Bi. Limilabo pia ameyahimiza makundi hayo maalumu kuhakikisha yanajisajili katika mfumo wa ununuzi wa umma ili kupata fursa ya kushiriki katika zabuni zinazotangazwa na serikali.

Aidha, amewataka kuwa tayari kuchukua hatua stahiki pale wanapoona hawajatendewa haki katika mchakato wa zabuni, kwa kuwasilisha malalamiko na rufaa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa ili kusaidia serikali kupata thamani halisi ya fedha katika utekelezaji wa miradi yake na kuhakikisha wananchi wananufaika na miradi hiyo kwa wakati uliopangwa.

# HABARIPICHA




*Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Anne Makinda akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba.*




*Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Laurent Deogratius Luswetula (Mb.) akiskani QR-Code inayoonesha huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba.*



*Sehemu ya washiriki wakifutilia mada kuhusu utatuzi wa migogoro, haki na usawa kwa wote katika michakato ya zabuni za umma katika Kongamano la Viwanda, Uwekezaji, Teknolojia na Uvumbuzi kwa Wanawake, Vijana, Wazee na Watu Wenye Mahitaji Maalumu wa mikoa ya Kanda ya Kusini lililoratibiwa na Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) mkoani Lindi, Septemba 2026.*